**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Wilayah Sudan**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿ وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ ﴾

**Jumamosi, 21 Rajab 1447 H** | **10/01/2026 M** | **Na: HTS 1447 / 78**


**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

# Hizb ut Tahrir / Wilayah Sudan Yafanya Visimamo Kadhaa katika Miji Tofauti Tofauti kote nchini Sudan

(Imetafsiriwa)

Ndani ya muundo wa mnasaba wa kumbukumbu ya miaka 105 ya kuvunjwa kwa Dola ya Khilafah mnamo Rajab 1342 H, na kama ukumbusho kwa Ummah wa tukio hili chungu, si kwa lengo la kulia juu ya historia tukufu iliyopotea, bali ili kuchochea azma ili Ummah uweze kutimiza wajibu wake wa kusimamisha Khilafah ili kuishi chini ya sheria za Mola wa Mlezi Walimwengu na kuondoa dhambi ya kifo cha Jahiliyyah kutoka shingoni mwake, Mashababu wa Hizb ut Tahrir katika Wilayah Sudan walifanya matembezi kadhaa katika miji tofauti kote Sudan, kufuatia swala ya Ijumaa mnamo 20 Rajab 1447 H, sawia na 9 Januari 2026 M, kama ifuatavyo:

• **Port Sudan**, mji mkuu wa utawala, mbele ya Msikiti wa Dhu al-Nurayn katika kitongoji cha Transit, ambapo ilihutubiwa na **Ustadh Ya'qub Ibrahim**, mwanachama wa Hizb ut Tahrir.

• **Mji wa Rabak** katika Jimbo la White Nile, mbele ya Msikiti wa Al-Taqwa.

• **Mji wa Al-‘Abbasiyyah Taqali** katika Jimbo la Kordofan Kusini, mbele ya Msikiti wa Al-Fuwailah katika kitongoji cha soko.

• Mji wa Al-Obeid, mji mkuu wa Jimbo la Kordofan Kaskazini, mbele ya Msikiti wa Soko la Ibn Mas’ud, ambapo ilihutubiwa na **Ustadh Muhammad Quni Muhammad**, mwanachama wa Hizb ut Tahrir.

**Khartoum Kaskazini (Bahri)**, mbele ya Msikiti wa Quba’ huko Al-Darushab.

• **Mji wa Omdurman**, mbele ya Msikiti Mkuu katika Soko la Sabreen, ambapo ilihutubiwa na **Ustadh Ahmad Abkar**, **wakili**, mjumbe wa Baraza la Hizb ut Tahrir katika Wilayah Sudan.

• M**ji la Al-Qadarif**, mji mkuu wa Jimbo la Al-Qadarif, kando ya Msikiti wa Abdul Qadir Abdul Muhsin (Reli) katika soko kuu.

Mashababu walikuwa wamebeba mabango yaliyoelezea tukio hilo na kufafanua umuhimu wa kuishi chini ya kivuli cha Khilafah. Wahudhuriaji walifanya maingiliano na visimamo hivi kwa njia ambayo inathibitisha hamu ya Ummah ya kurudi kwa Khilafah, ambayo kupitia hiyo kuna heshima yake na radhi ya Mola wake Mlezi.

**Ibrahim Othman (Abu Khalil)**
**Msemaji Rasmi wa Hizb ut Tahrir**
**katika Wilayah Sudan**


**Simu:** 0912240143- 0912377707

**Pepe:** Spokman_sd@dbzmail.com

**Tovuti:** www.hizb-sudan.org

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.org

**Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:** www.hizb-ut-tahrir.info